Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

**Swiss Agency for Development and Cooperation SDC**

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania



# MRADI WA KULETA MAGEUZI KATIKA SEKTA YA MKAA TANZANIA (TTCS)

## SHUHUDA ZA WANUFAIKAJI

Novemba 2019

## KUHUSU MRADI WA KULETA MAGEUZI KATIKA SEKTA YA MKAA TANZANIA (TTCS)

Mradi wa TTCS unatekelezwa na Mashirika matatu, Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) na Shirika la Kuendeleza Nishati Asilia Tanzania (TaTEDO).

Mradi una lengo kuu la kuhakikisha kuna mageuzi yanayozingatia uhimili wa mabadiliko ya tabianchi na uendelezaji wa watu maskini katika biashara na usimamizi wa mnyonyoro wa thamani wa mkaa na mazao mengine ya msitu. Mradi wa TTCS unakusudia kufikia lengo lake kupitia matokeo makuu mawili yanayotegemeana:

**Tokeo la 1:** Uendelevu na usimamizi bora wa mnyororo wa thamani wa mkaa na mazao mengine ya misitu inaboresha maisha ya watu vijijini, inaongeza uhimili wa mabadiliko ya tabianchi na kuboresha huduma za jamii katika wilaya tatu.

**Tokeo la 2**: Uwepo wa sera, sheria na miongozo inayozingatia usimamizi endelevu wa misitu na mazingira pamoja na watu maskini katika mnyororo wa thamani wa mkaa na mazao mengine ya misitu Awamu hii ya pili ya utekelezaji wa mradi ilianza mwaka Desemba 2015 na itaisha Novemba 2019.

Inatekelezwa katika vijiji 30 katika Wilaya 3 za Mkoa wa Morogoro: Kilosa, Mvomero na Morogoro. Shughuli za Mawasiliano, Uraghabishi pamoja na kujengea uwezo zinatekelezwa katika ngazi ya kitaifa.

Juhudi zimefanyika kuhakikisha kwamba taarifa na ushuhuda uliopo ndani ya kijitabu hiki zinatoka kwenye vyanzo vyenye uhakika na washiriki kutoka uwandani. Mfadhili ya mkusanyiko wa taarifa hizi (SDC) hausiki kabisa na mapungufu au maelezo yoyote.



Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

TaTEDO

MJUMITA

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

# MRADI WA KULETA MAGEUZI KATIKA SEKTA YA MKAA TANZANIA (TTCS)

## SHUHUDA ZA WANUFAIKAJI

**Novemba 2019**

# CONTENTS


UTANGULIZI 3

MAISHA BORA KUPITIA UCHOMAJI ENDELEVU WA MKAA 5

TAMBUA DHANA POTOFU KUHUSU WANAWAKE NA UZALISHAJI ENDELEVU WA MKAA 5

UVUNAJI ENDELEVU WA MBAO UNAVYOFANYA MAAJABU KATIKA HIFADHI YA MSITU WA IHOMBWE, WILAYA YA KILOSA 7

UTEKELEZAJI WA SHERIA NDOGO PAMOJA NA VITENDEA KAZI VYAONGEZA ARI YA USIMAMIZI WA RASLIMALI MISITU 9

VIONGOZI WENYE ARI, UJUZI NA MAARIFA KUSHIRIKISHA JAMII KUHUSU MAENDELEO ENDELEVU – KIJIJI CHA ULAYA MBUYUNI NA MAHARAKA 10

KILIMO HIFADHI CHA SAIDIA WAKULIMA WADOGO KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI 12

KUTOKA MIKOPO YA KILIMO CHA MPUNGA HADI KUWA MTUMISHI- NAMNA MIPANGO YA KUWEKA NA KUKOPA KIJIJINI KWETU ILIVYOINUA KILIMO NA ELIMU YA WANANGU" 13

BAADHI YA MASOMO- HUWAPA FURSA ZA KUKUA KIUCHUMI, "KUTOKA UCHOMAJI MKAA HARAMU MPAKA KUWA KAMPUNI YA BOSS KUKU" USHUHUDA WA BALAT 15

NDIYO, MAHUDHURIO YA MANAFUNZI DARASANI LAKINI MAZINGIRA YA KUJIFUNZIA HUONGEZA UFAULU WA WANAFUNZI!- SHULE YA MSINGI MATULI, WILAYA YA MOROGORO 16

KUJIAMINI ZAIDI KATIKA USALAMA WA AFYA KUPITIA MFUKO WA AFYA WA JAMII, SHUKURANI KWA USIMAMIZI WA MISITU ENDELEVU KATIKA KIJIJI CHETU 18

USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA JAMII – FURSA ISIYOONEKANA YA CHANZO CHA MAPATO ENDELEVU KWA HALMASHAURI ZA WILAYA 19

KUBORESHWA KWA UFUGAJI NYUKI KUMEONGEZA KIPATO CHA KAYA: 20

KUHUSU WABIA WA MRADI 22

## UTANGULIZI



Tangu mwaka 2012, Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) na Shirika la Kuendeleza Nishati Asilia Tanzania (TaTEDO), wametekeleza mfumo wa kuwezesha Usimamizi endelevu wa Misitu kwa kuingiza dhana ya uzalishaji endelevu wa mkaa kwenye Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (CBFM) kwenye misitu aina ya Miombo katika Wilaya za Kilosa, Mvomero na Morogoro, Mkoa wa Morogoro. Kwa njia hiyo manufaa mengi yamepatikana ikiwa ni kuboresha Uhifadhi wa Misitu ya vijiji, kuwekeza kwenye maendeleo ya jamii na kuongeza kipato kwenye serikali za vijiji na Halmashauri pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Mfumo huu ulikuwa na dhumuni la kuongeza motisha kwa jamii kuendelea kusimamia misitu yao kwa njia endelevu.

Mkusanyiko wa taarifa hizi kutoka kwa baadhi ya wanajamii unaturudisha nyuma kidogo toka mwanzo wa utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya mkaa Tanzania (TTCS) ambapo kwa miaka minne iliyopita toka Desemba 2015 hadi Novemba 2019, na kwa kujivunia mafanikio yaliyopo ambayo yamewezeshwa kupitia Ufadhili mkubwa wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC), mradi umeweza kuuonesha na kuthibitisha matokeo na mafanikio mengi katika nyanja mbalimbali ikiwemo mifano michache kama vile; kupunguza kiwango cha upotevu wa misitu katika vijiji vya mradi ukilinganisha na vijiji nje ya mradi kati ya mwaka 2014 na 2017 kilikuwa -1.64%, upungufu wa asilimia 29.9% ukilinganisha na mwaka 2010-2014; vijiji 30 vimeweza kuingiza dhana ya uzalishaji mkaa kwa njia endelevu kwenye usimamizi wa misitu yao ya vijiji na kuongeza mapato ya vijiji na wazalishaji kufikia zaidi ya Dola za kimarekani 599,675 kufikia mwisho wa mwaka 2018; vijiji 28 vina mipango ya matumizi bora ya ardhi, wameanda mipango ya usimamizi wa misitu yao ya vijiji pamoja na sheria ndogo na mipango ya uvunaji endelevu wa misitu yao kwenye ardhi za vijiji. Uwelewa umeongezeka sana miongoni mwa wadau kuhusu usimamizi wa nishati tungamotaka hivyo kuongeza mijadala na mikakati katika ngazi mbalimbali. Pia uwezo umejengwa kwa wadau katika ngazi mbalimbali wa nanma ya kusaidia jamii kuingiza dhana hii kwenye Usimamizi wa Misitu ya vijiji. Kwa wakati wote, ushirikishwaji na ujumuishwaji wa kina mama, kina baba, vijana na makundi yote ndani ya jamii umezingatiwa katika kupanga, kutekeleza na kunufaika na manufaa ya mradi kwenye vijiji, hivyo kuboresha utawala bora.

Mradi umefanya kazi na vijiji 30 ndani ya wilaya za Morogoro, Kilosa and Mvomero, umeshirikisha Halmashauri za Wilaya, na viongozi wake pamoja na wawakilishi wa wananchi. Pia umeshirikisha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, pamoja na Asasi zisizo za serikali, Wanazuoni, wanahabari pamoja na watunga sera.

Ukusanyaji na utayarishaji wa kijitabu hiki chenye shuhuda mbalimbali kutoka kwa wananchi na wanufaikaji wa shughuli za mradi umeangalia mabadiliko yanayochangia matokeo chanya kupitia shughuli za mradi wa wananchi na watekelezaji pamoja na wadau wa mradi.

Mkusanyiko huu wa taarifa unadhamiria kuonesha uzoefu na ushuhuda wa wanufaikaji ambao wameona thamani ya ushiriki wao katika mradi. Hajujaweza kuwafikia shuhuda zote zilizopo lakini tuna imani utaweza kupitia kurasa nyingine za mitandao ya kijamii kwa ajili ya taarifa zaidi za mradi. Ni matumaini yangu kuwa shuhuda hizi zitachangia kubadilisha mtizamo wa namna watu wanavyosimamia rasilimali zao kwenye ardhi za vijiji na kuendeleza ushiriki wa jamii katika kusimamia na kuongeza mjadala kuhusu umuhimu wa usimamizi endelevu wa misitu ya jamii nchini.

**Charles Meshack**
Mkurugenzi Mtendaji,
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG).



***Bw. Rashidi kutoka Kijii cha Ulaya Mbuyuni katika tanuru lake akiangalia maendeleo ya mkaa kama bado unawaka.***



***Bi. Amina Ally Mohamed kutoka kijiji cha Mlilingwa, akifanya kazi kwenye tanuru lake baada ya kupokea mafunzo kuhusu namna ya uzalishaji endelevu wa mkaa.***

## MAISHA BORA KUPITIA UCHOMAJI ENDELEVU WA MKAA

*Bw. Rashid Kazeuka ni mojawapo wa wazalishaji wa mkaa endelevu katika kijiji cha Ulaya Mbuyuni, Wilaya ya Kilosa, anasema; "kabla ya kuja kwa mradi katika kijiji chetu, tulikuwa tukichoma mkaa kwa kutumia mbinu za kienyeji ambapo tulipata mkaa wa kiwango cha chini na kukata miti mingi. Mradi umetoa mafunzo ya namna ya bora ya kuzalisha mkaa bila kuharibu misitu. Kwa tanuru la kisasa natumia siku tatu tu badala ya siku kumi nilizokuwa natumia kwa mbinu ya kienyeji. Kipato changu kimeongezeka, kwa sasa ninakidhi mahitaji ya familia yangu. Kwa sasa familia yangu inapata milo mitatu kwa siku nikilinganisha na zamani, na mke wangu anaweza kwenda buchani kama wanavyofanya wake wa watumishi wa umma. Pia, nimekuwa na uwezo wa kumpamba mke wangu, na watoto wangu wanakwenda shule wakiwa wamevaa sare safi na viatu.*


***Uzalishaji endelevu wa mkaa ni mfumo unatotumika kuzalisha mkaa katika misitu ya vijiji chini ya usimamizi shirikishi wa misitu unaozingatia kanuni za uvunaji kiikolojia. Mfumo wa uvunaji uliochukuliwa katika vijiji teule vyenye misitu wa mkaa kwa uvunaji wa mzunguko wa miaka 24 katika kipimo cha mita 50 kwa 50 hujulikana kama Eneo Dogo la uvunaji (EDU). Mradi wa Mkaa endelevu unatumia teknolojia ya tanuru Kichuguu Udongo la Kifusi lililoboreshwa na hivyo kutoa mkaa uliobora. Umri wa mzunguko wa miaka 24 unatumika kuhakikisha uendelevu wa misitu. Miti yenye kipenyo pungufu ya 15sm, miti ya mbao na matunda, makazi kwa wanyama na madhari haikatwi.***

## TAMBUA DHANA POTOFU KUHUSU WANAWAKE NA UZALISHAJI ENDELEVU WA MKAA

Bi. Amina Ally Mohamed kutoka kijiji cha Mlilingwa, Kata ya Ngerengere, Wilaya ya Morogoro, anasema *"Ninashukuru sana kwa Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS) kwa kuwa umeniwezesha kuwa mmoja wa wazalishaji wa mkaa wanaotumia mbinu zilizoboreshwa ambazo ni rafiki wa misitu na mazingira. Licha ya kuwapo kwa dhana potofu kuhusu wanawake kuwa hawawezi kufanya kazi ngumu ambazo wanaume wanafanya, ninajivunia kwamba ninafanya kazi hii kwa weredi baada ya kuhudhuria mafunzo ambayo yaliendeshwa na mradi. Mimi ni mmojawapo wa watu wanaofanya kazi hii kwa ufanisi ambapo mpaka sasa nimeshatengeneza matanuru kumi. Aidha kwa sasa ninaweza kusaidia wengine ikiwa ni pamoja na wanaume kuandaa tanuru. Ninajivunia na biashara hii kwa sababu sasa ninaweza kumudu gharama za elimu kwa watoto wangu; kushiriki kwa ufanisi katika vyama vya kuweka na kukopa ambapo ninaweza kukopa fedha na kufanyia shughuli zingine kama vile kupanua shamba langu. Nimeanzisha ufyatuaji wa matofari, na nimatumaini yangu kuwa mwaka ujao kwa kushirikiano na mume wangu tutaweza kujenga nyumba ya kisasa kwa familia yetu".*



*Bi. Varshty Chimile, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Ihombwe, akiwa amesimama mbele ya nyumba anayoishi, iliyojengwa kutokana na mapato yaliyokusanywa kutokana na uendeshaji wa mradi wa Uchomaji endelevu wa mkaa na mbao katika kijiji chake.*



*Wanachama wa chama cha uvunaji mbao endelevu cha Ihombwe wakifanya kazi pamoja katika kupanga mbao baada ya uvunaji tayari kwa kuuza.*


## UVUNAJI ENDELEVU WA MBAO UNAVYOFANYA MAAJABU KATIKA HIFADHI YA MSITU WA IHOMBWE, WILAYA YA KILOSA

Bi. Varshty Chimile, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Ihombwe anasema; *"uvunaji endelevu wa mbao umekuwa mojawapo ya vyanzo vikuu vya mapato katika eneo lao. Mwezi Mei, 2019, tulisaini mkataba na* ***Kampuni ya mbao ya*** *Tabora kuzalisha mita za ujazo1755 za slipa za mbao kutumika katika shughuli za ujenzi wa Reli mpya (Standard Gauge Railway- na ukarabati wa Reli ya Tanga – Moshi. Awamu ya kwanza ya mita za ujazo mia moja hamsini na tano (155m)$^3$ zimenunuliwa kwa jumla ya shilingi za kitanzania 47,000,000 kama mapato ya kijiji, asante kwa Usimamizi Shirikishi wa Misitu. Awamu ya pili yenye mita za ujazo1600 itahitajika kuvunwa mapema Julai mwaka 2019, ambapo kijiji kinatarajia kupata jumla ya shilingi. 240,000,000. Kwa hakika, biashara hii inalipa, hatukuwahi kuchukulia misitu kama rasilimali endelevu kwa ajili ya kijiji na kijiji chetu kwa sasa kinasonga mbele katika maendeleo kupitia misitu. Kijiji kimekuwa na uwezo wa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia mapato haya ikiwemo ujenzi wa madarasa matatu (mawili shule ya msingi Ihombwe na moja Mbegesela), kuweka umeme katika ofisi za kijiji, madarasa na nyumba za wafanyakazi wa shule ya msingi Ihombwe na Zahanati" (ikiwemo nyumba ninayokaa mimi mtendaji).*

> ***"Sisi kama viongozi wa kijiji kupitia kamati ya Maliasili ya kijiji tutahakikisha kwamba kanuni zote za uvunaji endelevu wa mbao zinazingatiwa na kwa yeyote atakayekiuka taratibu zilizopo, atawajibika kwa kufuata sheria zetu ndogo".***

Zaidi ya hapo, Varshty anaongeza kuwa; *"tumekuwa na uwezo wa kujenga nyumba moja ya wafanyakazi katika Zahanati ya Ihombwe na kukarabati barabara ya kijiji yenye umbali wa takribani kilomita kumi na nane (18) kutoka njiapanda ya Kilosa – Mikumi. Kwa sasa barabara inapitika na imewezesha ufikikaji wa mjini Kilosa na Mikumi. Mradi huu umekuwa mmojawapo wa wabia wa maendeleo katika kijiji hiki, tuko maeneo ya kijijini, lakini staili ya maisha ni kama ile ya mazingira ya mjini kwa sababu ya upatikanaji wa huduma za msingi kwa kiwango kinachotakiwa. Sisi kama viongozi wa kijiji kupitia kamati ya Maliasili ya kijiji tutahakikisha kwamba kanuni zote za uvunaji endelevu wa mbao zinazingatiwa na kwa yeyote atakayekiuka taratibu zilizopo, atawajibika kwa kufuata sheria zetu ndogo".*





*Baiskeli na pikipiki zinazosaidia timu ya doria kufanya majukumu yake katika kuhakikisha kuwa maeneo ya misitu yanatunzwa na kulindwa vizuri. Hizi zinanunuliwa kutokana na mapato ya usimamizi endelevu wa misitu ya kijiji.*



*Bwana Juma Chelasa, mweka hazina wa Kamati ya Kijiji ya Maliasili katika Kijiji cha Ihombwe*






## UTEKELEZAJI WA SHERIA NDOGO PAMOJA NA VITENDEA KAZI VYAONGEZA ARI YA USIMAMIZI WA RASLIMALI MISITU

*Bw.* Juma Chelasa ni mweka hazina wa Kamati ya Maliasili ya kijiji cha Ihombwe anasema “*kabla ya Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS), uvunaji usio endelevu wa raslimali misitu ulikuwa kitendo cha kawaida katika kijiji chetu. Kamati ya Maliasili ya kijiji haikuwa na uwezo wa kusimamia raslimali za misitu. Baada ya Mradi kuanza tulipata mafunzo kuhusu usimamizi endelevu wa raslimali misitu. Kwa sasa kamati ina ufahamu wa wajibu na majukumu yake. Tuna jukumu la kukusanya mapato kutokana na maliasili za misitu na hizi zimesaidia serikali ya kijiji chetu kupanga miradi ya maendeleo yenye manufaa kwa jamii katika kijiji hiki. Kwa sasa kijiji kiko makini sana kuona sheria ndogo zinazoongoza matumizi ya maliasili zinazingatiwa. Ili kutekeleza majukumu kwa ufanisi, kijiji kimetenga 40% ya mapato yanayokusanywa kwa shughuli za usimamizi wa misitu. Hali hii imewezesha Kamati kuendesha doria ili kubaini shughuli zozote za kiharifu katika misitu. Kamati ina nyenzo za usafiri yaani baiskeli na pikipiki ambazo zinasaidia timu ya doria kutekeleza majukumu yake”.*

Zaidi ya hapo, Bw. Chelasa anaongeza “*tunafahamu kuwa ni vigumu kwa Kamati pekee kudhibiti vitendo vya kiharifu, kwa sababu hii, mbinu kuu ni ushirikiano na jamii, ukuzaji ufahamu na jumuiya ya wanachama kufahamu kazi zao katika kusimamia raslimali misitu. Mathalani, sheria zetu zinasema kazi na majukumu ya kila mtendaji kama vile serikali ya kijiji, Kamati ya Maliasili ya kijiji na jamii. Pia, sheria zinatoa faini kwa wakiukaji na motisha kwa watoa taarifa. Kwa sasa misitu ipo katika hali nzuri tangu kuanza kutekeleza mradi huu. Mapato kutokana na raslimali misitu yameongezeka na kijiji chetu kinanufaika*”.

# VIONGOZI WENYE ARI, UJUZI NA MAARIFA KUSHIRIKISHA JAMII KUHUSU MAENDELEO ENDELEVU – KIJIJI CHA ULAYA MBUYUNI NA MAHARAKA




***Baadhi ya wajumbe wa wa Halmashauri ya Kijiji na wajumbe wa Kamati ya Maliasili ya kijiji cha Ulaya Mbuyuni wakiwa katika picha ya pamoja mbele ya jengo la ofisi ya Kijiji.***

Bw. Omar Mlinga mwenyekiti wa kijiji cha Ulaya Mbuyuni Wilayani Kilosa, anasema: "kabla ya Mradi wa kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS), viongozi hatukujua wajibu na majukumu yetu. Mradi umetujengea uwezo *si tu stadi za uongozi, bali pia usimamizi endelevu wa raslimali za kijiji. Tumeweza kujenga madarasa, ofisi ya walimu na kijiji, na kuchimba kisima kirefu". Ufahamu wa wajibu na majukumu yangu kama mwenyekiti umeniwezesha kusimamia mambo ya kijiji katika namna ya shirikishi. Hivi sasa si tu tunaweza kutekeleza usimamizi endelevu wa raslimali zetu bali pia kijiji kinakusanya mapato zaidi kuliko ilivyokuwa kabla. Mtizamo umebadilika na kuongeza umiliki katika uendelevu wa miradi ya kijiji.*



Mwenyekiti wa kijiji cha Maharaka (katikati katika picha) kilichoko wilayani Mvomero, Bw. Mwichande Kibwana anasema: *“kujengewa uwezo katika stadi za uongozi na utawala kumeniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika namna ya uweledi zaidi. Ninafahamu umuhimu wa kufanya maamuzi ya pamoja, kushirikisha wanajamii na namna gani nzuri ya kusimamia raslimali za kijiji. Mikutano ya Serikali ya kijiji na mkutano mkuu wa kijiji hufanyika kulingana na mataka ya Sheria ya Serikali za Mitaa. Kwa sasa Jamii inaufahamu wa haki zake na kuzidai kama itanyimwa. Siku hizi wanajamiii wanadai taarifa ya mapato na matumizi. Kama utachelewa kuitoa, utalazimishwa kufanya hivyo, kwa sasa tunatoka kwenye mazoea ya kufanya kazi kama kawaida kwenda kwenye staili ya uongozi wa kuzingatia Sheria, taratibu na kanuni”.*

## KILIMO HIFADHI CHA SAIDIA WAKULIMA WADOGO KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI



***Mafunzo kuhusu Utunzaji wa kilimo huhusisha uandaaji wa shamba, matumizi ya mbegu bora, ukatuzi wa chini na namna gani ya kupanda. Matumizi ya mbolea kama vile samadi na mboji na umuhimu wa palizi mapema.***

***Bi. Salma Shabani kutoka kijiji cha Mlilingwa, akiwa amesimama katika shamba darasa la kijiji ni mmoja wa waliopewa mafunzo ya kilimo hifadhi***

Bi. Salma Shabani ni mmojawapo wa wakulima wadogowadogo katika kijiji chaMlilingwa aliyekuwa akikabiliwa na tatizo la kupata mavuno ya mazao kidogo karibia kila mwaka. Bi Salma anasema; *"chanzo kikubwa cha tatizo hilo ni pamoja na ardhi kukosa rutuba, uzalishaji mdogo, na usimamizi mdogo wa mashamba pamoja na utunzaji wa mazao baada ya kuvuna. Mradi wa TTCS ulihamasisha kilimo hifadhi kama mojawapo ya mkakati wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa ambacho kikizingatiwa si tu kinaongeza mavuno ya mazao kwa wakulima bali pia hutunza mazingira. Mradi uliandaa mafunzo kuhusu kilimo hifadhi kupitia Shamba Darasa la Wakulima. Tulikuwa wakulima 30 tuliopata mafunzo haya. Nimebaini kuwa kuna tofauti katika mavuno ya mazao, kabla ya mafunzo hayo, nilikuwa ninavuna magunia 6-8 ya kilo 90 kwa ekari, kwa kutumia elimu ya kilimo hifadhi kwa sasa ninavuna mpaka magunia 20 ya kilo 90 kwa ekari. Kwa sasa familia yangu ina chakula cha kutosha ambapo hapo awali haikuwa hivyo. Hakuna mashaka kabisa kama tunataka kuboresha maisha yetu kupitia kilimo tunapaswa kuachana kabisa na matumizi ya mbinu za kilimo cha kienyeji na kufuata kilimo cha kisasa kama vile kilimo hifadhi. Hii itasaidia kuinusuru misitu yetu pia".*

## KUTOKA MIKOPO YA KILIMO CHA MPUNGA HADI KUWA MTUMISHI- NAMNA MIPANGO YA KUWEKA NA KUKOPA KIJIJINI KWETU ILIVYOINUA KILIMO NA ELIMU YA WANANGU”



***Bibi Maliki akielezea historia yake kuhusu matokeo ya akiba ya kijiji na mpango wa mikopo katika maisha yake.***

Bibi Austeria Maliki wa kijiji cha Ihombwe ni mnufaika wa kilimo hifadhi na dhana ya kuweka na kukopa, anasema: “*nilihudhuria mafunzo ya kilimo hifadhi. Baada ya mafunzo, nilikopa shT. 300,000/= kutoka chama changu cha kuweka na Kukopa na nikanunua hekari moja ya ardhi ya mpunga ambayo iliniwezesha kuongeza uzalishaji wa mpunga. Pia, wakati wa kiangazi niliitumia ardhi hiyohiyo kulima nyanya na hivyo kuongeza kipato. Kipato nilichopata kilinisaidia kulipa ada ya mtoto wangu. Bila shughuli hizi, sidhani kama mtoto wangu sasa angekuwa mtumishi wa umma katika nchi hii. Ninashukuru kwa Mradi wa TTCS kunionesha njia ya kufanya*”



**Bw. *Metusi Mtevele katika shamba lake la miwa ambapo amekuwa na uwezo wa kumiliki baada ya kujiunga na Kikundi cha Kuweka na kukopa cha Tupendane kilichopo kijiji cha Ihombwe***

*Jina langu naitwa Metusi Mtevele mwanachama wa kikundi cha Kuweka na Kukopa cha Tupendane katika kijiji cha Ihombwe. Kabla ya kujiunga na chama, nilikuwa natunza fedha zangu sehemu ndani ya nyumba yangu kitu ambacho kilikuwa hatari sana. Wakati mradi unakuja, tuliambiwa kwamba tunaweza kutunza fedha ili tuweze kuzitumia wakati wa kipindi kigumu, tunaweza kuchukua mkopo kwa masuala ya maendeleo, Kwa hiyo, tulianzisha Kikundi cha kuweka na kukopa. Mwanzoni tulikuwa tunatunza fedha zetu katika sanduku la chuma. Tukagundua kwamba kutunza fedha kwenye sanduku hili ni hatari, Pia, ilikuwa ni hatari sana kwa mtu anayelitunza, tuliamua kufungua akaunti Benki. Siku hizi, tunatunza fedha zetu katika Benki na pia makusanyo kutoka kwa wanachama yanapelekwa moja kwa moja kupitia mfumo wa 'simubenki'. Nadhani tumepiga hatua na mnapaswa kutupongeza. Ninanufaika sana kuwa wanachama wa chama hiki. Nilichukua mkopo wa kwanza wa shT. 280,000/=, niliutumia kununua ardhi ya ukubwa wa ekari 1.25 ambayo niliitumia kulima mahindi mwaka 2014 hadi 2017. Kipindi cha 2017 na 2018, nilianzisha shamba la miwa lenye ukubwa wa ekari mbili. Matarajio yangu ni kuvuna tani 30 za miwa na kwa sasa bei iliyopo ni shilingi. 110,000/= kwa tani moja, hii inamaana kwamba ninatarajia kupata jumla ya shilingi. 3,300,000/=. Faida nyingine ninazojivunia ni kuona familia yangu ina furaha kwa kuwa tuna chakula cha kutosha na nina uwezo wa kulipia ada ya shule watoto wangu. Ninaujuzi wa kutosha na kikundi chetu kinazidi kuimarika hivyo nitaendelea na shughuli zangu kama kawaida kwa sababu nina uwezo na ninajiamini kuifanya.*

## BAADHI YA MASOMO- HUWAPA FURSA ZA KUKUA KIUCHUMI, "KUTOKA UCHOMAJI MKAA HARAMU MPAKA KUWA KAMPUNI YA BOSS KUKU" USHUHUDA WA BALAT

Kijiji cha Mlilingwa kimejaliwa kuwa na rasilimali misitu. Kipindi cha nyuma, shughuli haramu zilifanyika katika misitu ikiwa ni pamoja na uchomaji mkaa ulioshamiri kiasi cha kutishia uwepo wa misitu. Mradi wa TTCS ulihamasisha uanzishaji wa usimamizi shirikishi wa Misitu na kutoa mafunzo kwa wanakijiji kuhusu mbinu za uzalishaji endelevu mkaa. Bw. Balati Latilali Patel alimaarufu kwa jina la "Zungu" alikuwa mmoja wa wachoma mkaa haramu ambaye alihudhuria mafunzo. Bw. "Zungu" anasema *"nilihudhuria mafunzo pamoja na marafiki zangu 12. Tulifunza kuhusu namna endelevu ya kuandaa mkaa, baada ya mafunzo tulianza kuchoma mkaa kwa kutumia mbinu tulizojifunza. Tulikubaliana kuchanga shilingi 10,000/= kila mwezi kama akiba yetu. Baada ya kutunza akiba kwa muda wa mwaka mmoja tulikusanya jumla ya shT. 1,200,000/=, kwa fedha hizi, tuliamua kuanzisha biashara ya kufuga kuku ambapo tulianzisha kikundi chetu kilichoitwa "Boss kuku". Tulijenga banda la kuku lenye kuchukua kuku 300, tulinunua vifaranga 300 kwa bei ya shT. 1,500/= kila kifaranga. Kupitia kuuza kuku na mazao mengine kama vile mayai na mbolea ya kuku, tuliweza kujenga banda lingine lililokuwa na uwezo wa kuchukua kuku 1000 ambao waligharimu shT. 16,000,000/=.*

*Baada ya kujenga banda jipya tuliamua kununua mashine ya kukutolesha cha gharama ya shilingi 1,500,000/=. Mashine hii ya kutotolesha iliufanya ufugaji wetu kuwa wa ufanisi zaidi kwa kuwa tunazalisha vifaranga wenyewe. Kwa sasa tunauza kuku, mayai, na mbolea. Bei kwa kuku ni kati ya 15,000/= hadi 20,000/= kutegemea na ukubwa wa kuku. Kwa kuku 1000 tunapata kati ya million 15-20- kwa kila miezi sita. Hakuna mashaka kuwa kama isingekuwa mradi huu, tusingeweza kufika mbali. Kikundi cha Boss kuku kimeonesha njia ya namna ya kubadili mtazamo unaweza kumgeuza mtu kuwa na maisha mazuri na kwa sasa hatushiriki tena katika shghuli ya uchomaji mkaa.*




*Bw. Balati Latilali Patel kutoka kikundi cha Boss Kuku katika kijiji cha Mlilingwa akiwapa kuku chakula. Kikundi hiki kilianzishwa kutokana na mapato ya kutoka kwenye uchomaji wa mkaa endelevu.*



*Bw. Balati Latilali (katibu wa kikundi cha Boss kuku katika kijiji cha Mlilingwa) akionesha kitotoa cha kikundi cha Boss kuku.*

## NDIYO, MAHUDHURIO YA MANAFUNZI DARASANI LAKINI MAZINGIRA YA KUJIFUNZIA HUONGEZA UFAULU WA WANAFUNZI!- SHULE YA MSINGI MATULI, WILAYA YA MOROGORO.



*Madarasa yenye umeme wa Jua ambayo huwasaidia wanafunzi kujisomea wakati wa usiku yamewezeshwa na mapato yanayotokana uzalishaji mkaa endelevu.*

Shule ya msingi Matuli ni mojawapo ya shule za msingi katika Wilaya ya Morogoro. Shule ilikuwa na changamoto mbalimbali si tu ziliathiri mazingira ya ujifunzaji bali pia matokeo ya wanafunzi. Serikali ya kijiji kupitia kamati ya shule iliamua kuwekeza sehemu ya mapato inayotokana na misitu yake ili kuboresha miundombinu ya shule kwa lengo la kuongeza mazingira mazuri ya ujifunzaji na kuanzisha programu za mafunzo ya ziada kuboresha matokeo ya wanafunzi. Kijiji kilitenga fedha kukarabati madawati na madarasa. Juu ya hayo, vilijengwa vyoo vya kisasa vya wanafunzi matundu 16 na matundu 2 ya walimu, mfumo wa uvunaji maji wa matanki mawili ya maji na mengine kwa walimu, mabadiliko haya yameboresha mazingira ya ujifunzaji shuleni.



Shakira Omari, mwanafunzi wa darasa la saba katika shule ya msingi ya Matuli anasema: "*ninasoma kwa umakini zaidi ili nifaulu mitihani yangu na siku moja niwe daktari. Hakuna sababu ya kwanini nishindwe mtihani ilihali tuna mazingira mazuri ya kujifunzia, walimu wenye motisha na muda mzuri wa maandalizi ya mtihani*"

Bi. Emma Daud Sanga ni mojawapo wa walimu wa shule ya msingi Matuli anasema*: "shule yetu ilianzisha programu ya kina kuandaa wanafunzi wa darasa la saba kwa mtihani wao wa taifa. Programu iliendeshwa kwa miezi miwili kuanzia Julai hadi Septemba kabla ya mtihani.*

*Wanafunzi wote wa darasa la saba waliweka kambi shuleni ambapo walisoma mchana na usiku. Hii iliwezekana kwasababu kamati ya shule ilipokea fedha kutoka kijijini kuboresha miundombinu kama vile uwekaji wa umeme. Kijiji kilisaidia programu hii kwa kugharimia chakula cha wanafunzi, ingawaje wazazi walichangia kidogo lakini kiwango kikubwa kilitolewa na kijiji. Tumeona matokeo ya programu hii kupitia matokeo ya kitaaluma na kiwango cha ufaulu cha wanafunzi. Mathalani, mwaka 2016, mwanafunzi mmoja tu alifaulu mtihani wa darasa la saba lakini baada ya kuanzisha programu ya kambi shuleni, mwaka 2017 wanafunzi 49 kati ya 53 walifaulu (ambapo wavulana walikuwa 24 na wasichana 25) na mwaka 2018 wanafunzi wote walifaulu. Mafanikio yote haya yamepatikana kwa sababu sasa tunafanya kazi katika mazingira mazuri yenye motisha kwa wanafunzi na walimu".*





***Bi. Amina Ali Mohamed kutoka kijiji cha Mlilingwa, kata ya Ngerengere, wilaya ya Morogoro pamoja na mume na mtoto wake akifurahia kushika kadi ya Bima wa Afya wa Jamii CHF iliyoboreshwa.***

## KUJIAMINI ZAIDI KATIKA USALAMA WA AFYA KUPITIA MFUKO WA AFYA WA JAMII, SHUKURANI KWA USIMAMIZI WA MISITU ENDELEVU KATIKA KIJIJI CHETU


Uwezo wa kumudu gharama za matibabu ya afya ni mojawapo ya masuala yanayoathiri watu wengi kijijini. Baadhi ya wagonjwa wanakufa kwa sababu hawawezi kumudu gharama za matibabu. Hakuna mashaka kabisa kama utaratibu ukiwekwa wa bima ya afya, watu wataongeza muda wa kujiamini katika maisha yao. Mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Mkaa Tanzania umehimiza serikali ya kijiji kujiunga na mpango wa afya wa jamii ili jamii iweze kuongeza kujiamini katika maisha yao. Vijiji vyote katika maeneo ya mradi vilijiunga na Mpango wa afya wa jamii, na sasa watu wanapata matibabu kupitia bima ya afya.

Bi. Amina anasema: *"mojawapo ya jambo la ajabu ambalo sitalisahau katika maisha yangu ni kijiji kulipa ada ya uanachama kwa mfuko wa afya wa jamii ulioboreshwa. Mimi, mume na mtoto wangu tunafurahia mafanikio haya kwa kuwa hatuna wasiwasi kuhusu gharama za matibabu wakati mmoja wetu anapougua, Mathalani, siku moja mtoto wangu aliugua nilikwenda Ngerengere kupata matibabu. Nilitumia takribani siku kumi hospitalini lakini nilitumia kadi ya bima ya afya tu. Nina uhakika kama kusingekuwapo na utaratibu huo, sifahamu hali ingekuwaje kwa mtoto wangu, Shukurani kwa wote waliofikiria kuwa na kadi hizi. Kwa sasa tunaweza kutumia fedha ambazo zingetumika kwa matibabu ya afya katika shughuli nyingine za uzalishaji kujipatia kipato katika familia zetu"*.

# USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA JAMII – FURSA ISIYOONEKANA YA CHANZO CHA MAPATO ENDELEVU KWA HALMASHAURI ZA WILAYA

Wilaya ya Kilosa ni mojawapo ya wilaya katika nchi ambazo zimejaliwa kuwa na raslimali za misitu ya kutosha. Hatahivyo, wilaya kwa miaka mingi haijafaidika na mapato yatokanayo na misitu kwa sababu ya usimamizi dhaifu wa raslimali za misitu. Mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Mkaa Tanzania kwa ushirikiano na wilaya ulijikita katika kujenga uwezo wa jamii kusimamia raslimali misitu kupitia Usimamizi wa Misitu Shirkishi Jamii. Bw. John Mtimbanjayo Mratibu wa MradI upande wa Wilaya ambaye pia ni Afisa Maliasili Wilaya anasema: "*Usimamizi wa Misitu Shirikishi Jamii umeimarisha usimamizi wa raslimali wa misitu ambapo takribani hekta 114,690 za misitu ya asili zimeweza kuhifadhiwa. Aidha, usimamizi wa raslimali wa misitu, vijiji vimeweza kuongeza mapato ya kijiji ambayo yamekuwa yakitumika katika kugharimia miradi ya jamii kwa vipaombele vyao hivyo, kumpunguzia mzigo Mkurungezi Mtendaji wa Wilaya*. *Baadhi ya miradi ya jamii ambayo imekuwa ikigharimiwa kupitia mapato ya kijiji ni: kujenga madarasa na ofisi za walimu; kulipia mipango ya afya ya jamii kwa wanakijiji wote kwa baadhi ya vijiji; kuchimba visima vya kina kirefu; kukarabati zahanati za vijiji; kujenga nyumba za walimu na madaktari; kulipa posho za walimu wa kujitolea; kukarabati mtandao wa barabara wa takribani kilomira 19 kwa kutaja chache. Zaidi ya hapo, mapato ya misitu ya wilaya yameongezeka kutoka shilingi Millioni 65 kwa mwaka hadi million 335 ambazo zinalipwa na vijiji kama 10% ya kile vinavyopata kutokana na mauzo ya mazao ya misitu. Kuongezeka kwa mapato kumewezesha shughuli mbalimbali za maendeleo kufanyika na hivyo wilaya nayo kuanza utaratibu huo kwenye vijiji vingine.*

*Aidha, wilaya imekuwa ikipokea wageni mbalimbali wakiwemo viongozi wa kitaifa wanaokuja kujifunza kuhusu mafanikio yetu. Hakuna shaka kuwa kama Halmashauri zitawekeza kwa ufanisi katika* Usimamizi Shiriki jamii wa Misitu manufaa ya utunzaji wa raslimali misitu na uboreshaji maisha ya jamii utakuwa juu. Halmashauri ya wilaya ya Kilosa imejaribu mbinu hii na kwa sasa inanufaika zaidi. Kwa wale ambao watataka kujifunza zaidi jinsi haya yanavyotokea, tunawakaribisha Kilosa kujifunza na kuchota uzoefu juu ya mafanikio haya".



***Bw. John Mtimbanjayo, Afisa Maliasili Halmashauri ya Wilaya na Mratibu wa Mradi wa Mkaa Endelevu Wilayani Kilosa akiwa ofisini kwake.***

## KUBORESHWA KWA UFUGAJI NYUKI KUMEONGEZA KIPATO CHA KAYA:





***Bw. Paulo Mahimbi ni mmojawapo wa wanachama wa Kikundi ca Ufugaji Nyuki cha Singa, akiangalia mizinga ya nyuki ambayo pia ni msaada kutoka mradi wa TTCS.***

Jina langu naitwa *Paulo Mahimbi, mkazi wa kijiji cha Ihombwe katika wilaya ya Kilosa. Miaka kumi iliyopita nimekuwa nikifuga nyuki, nilitumia mizinga ya nyuki ya kienyeji lengo langu lilikuwa kupata asali kwa matumizi ya nyumbani kwangu tu. Kuuza asali haikuwa kawaida yangu kwa kuwa hakuna mtu angeweza kununua asali. Mwaka 2014, mradi wamageuziya Sekta ya Mkaa Tanzania* ulinikaribisa kuhudhuria mafunzo ya uboreshaji ufugaji nyuki. Mafunzo yalikuwa mazuri na baada ya mafunzo hayo, tuliunda kikundi cha wafugaji nyuki tulichokiita Singa. Tulianza na mizinga ya nyuki mitano ambayo ilitolewa na *mradi.* Mpaka sasa kikundi chetu kina mizinga ya nyuki 25, tunavuna asali mara tatu kwa mwaka na kila mwanachama anapata mapato ya shilingi 180,000/= kila tukivuna; inamaanisha kuwa kwa mwaka, kila wanachama anapata shilingi 540,000/=. Mimi *nilitunza pesa mpaka nilipofikisha shilingi 540,000/= ambazo nilinunua magunia 25 ya mahindi. Baada ya miezi mitano niliuza mahindi na kupata mara tatu ya pesa niliyowekeza. Huu ulikuwa mwanzo wa mimi kuboresha maisha yangu. Nilipanua biashara yangu kwa kuwa nilikuwa na mtaji wa kununua mahindi zaidi. Mpaka sasa ni mmojawapo wa watu unaoweza kuwahesabu katika kijiji hiki waliopata mageuzi katika maisha yao. Nilijenga nyumba na kuweka umeme, kwa sasa familia yangu ina akiba ya chakula na upatikanaji wa mahitaji muhimu. Sitasahau ufugaji wa nyuki kwa kuwa ninaamini kwamba ulikuwa msingi wangu wa mafanikio wa haya yote. Mungu, asante kwa kuruhusu* Mradi wa TTCS kufanya kazi na sisi”.


HALMASHAURI YA KIJIJI CHA ULAYA-MBUYUNI
KIJIJI HIKI KINATEKELEZA MPANGO
WA MATUMIZI BORA YA ARDHI
USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU
PAMOJA NA MKAA ENDELEVU
Ni Marufuku:
• KUCHOMA MOTO HOVYO
• KUFYEKA/KUHARIBU MISITU
• KUHARIBU VYANZO VYA MAJI
TUNZA MAZINGIRA ILI NAYO YAKUTUNZE
"MAZINGIRA NI UHAI"



## KUHUSU WABIA WA MRADI

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

**Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC)-** SDC ni Shirika la kimataifa la maendeleo na ushirikiano kutoka Uswisi lililoko kwenye Idara kuu ya Mambo ya Nje (FDFA). Mradi unafadhiliwa na SDC. daressalaam@eda.admin.ch www.eda.admin.ch/daressalaam

**Wabia watekelezaji:**

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

**Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG)-** TFCG ni shirika lisilo la kiserikali nchini lenye maono ya kuhifadhi na kurejesha baioanuwai za misitu yenye umuhimu wa kimataifa Tanzania. TFCG ni mtekelezaji mkuu wa mradi. tfcg@tfcg.or.tz www.tfcg.org

**Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA)** -MJUMITA ni mjumuiko wa kitaifa wa mitandao ya jamii inayojihusisha na usimamizi shirikishi wa misitu. Mtandao unatoa jukwaa la kujengea uwezo, ushawishi na mawasiliano kwa ajili ya mitandao hii. MJUMITA inajihusisha kufanya ushawishi kuhusu sera ambazo zinatoa motisha katika usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii kwa kuingiza uzalishaji endelevu wa mkaa. mjumitaorg@mjumita.org www.mjumita.org

**Shirika la Kuendeleza Nishati Asilia Tanzania (TaTEDO)**- TaTEDO ni shirika linalojihusisha na maendeleo ya nishati endelevu ikiwa na uzoefu wa zaidi ya miaka 20 wa masuala ya nishati vijijini. TaTEDO inachangia kutekeleza mradi katika shughuli za uraghibishi na mawasiliano juu ya nishati endelevu ya tungamotaka katika ngazi ya kitaifa. energy@tatedo.org www.tatedo.org